

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



**TAARIFA KWA UMMA**

**VIJANA WANAOHITIMU VYUO WATAKIWA KUZITUMIA FEDHA  
ZINAZOTENGWA NA HALMASHARI KUJIONGEZEA KIPATO**

Serikali imewataka wahitimu wa vyuo mbalimbali nchini kuhakikisha wanatumia fursa ya uwepo wa fedha zinazotengwa na Halmashauri katika Wilaya zote nchini kila mwaka kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake kiuchumi.

Rai hiyo imetolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Dkt. Khatibu Kazungu, kwa niaba ya Waziri wa Wizara hiyo Mhe. Philip Isdor Mpango, wakati wa Mahafali ya 32 ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) Kanda ya Ziwa Jijini Mwanza.

Dkt. Kazungu alisema kuwa, Halmashauri zote nchini hutenga asilimia tano ya mapato yake ya ndani kila mwaka ili kuwawezesha vijana na wanawake kutumia fedha hizo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo na kuwataka wahitimu wa vyuo ambao hawana ajira katika Sekta rasmi, waanzishe vikundi vya umoja wa uzalishaji mali ikiwa ni moja ya kigezo cha kuweza kupata fedha hizo.

“Serikali ya Awamu ya Tano imejidhatiti kuwaletea wananchi maendeleo endelevu kwa kuhakikisha kila mtu kwa nafasi yake anafanya kazi uzalendo, uadilifu, bidii na maarifa lakini pia kudumisha amani na mshikamano ili kuwa na maendeleo endelevu kwa manufaa ya kizazi hiki na kijacho.” alisema Dkt. Kazungu.

Aidha aliwataka Wahitimu hao kuchangamkia fursa ya mtengamano wa Afrika Mashariki kwa kupata ajira si tu ndani ya nchi na hata nje ya nchi kwa kuwa Wahitimu hao wamebahatika kuwa na elimu yenye ubora inayoweza kuingia katika ushindani ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa upande wake Kaimu Mkuu wa Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), Prof. Hozen Mayaya, ameishukuru Serikali kwa kufanya maboresho katika sekta ya Huduma za Jamii ikiwemo elimu ambayo imewezesha Taasisi za Elimu ya Juu kuwa sehemu bora ya kujifunzia.

Alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa chuo hicho miaka 39 iliyopita, hakijaacha kusimamia ubora wa elimu kwa kuzingatiaa miongozo na kanuni zilizowekwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE).

Mkurugenzi wa Chuo cha IRDP Kanda ya Ziwa Dkt. Benedict Kilobe, alisema kuwa Mahafali hayo yamefanyika kwa mara ya sita katika kituo cha Mwanza, ambapo jumla ya wanafunzi 1,203 wamehitimu mafunzo ya programu mbalimbali zinazotolewa na chuo hicho wakiwemo Wanaume 519 sawa na asilimia 43.1 na Wanawake 684 sawa na asilimia 56.9.

Mahafali ya 32 ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) Kanda ya Ziwa Jijini Mwanza yalikusisha Wahitimu wa ngazi ya Astashahada, Stashahada na Stashahada za Uzamili ambao walipata mafunzo kwa vitendo katika maeneo mbalimbali nchini ambayo yatawafanya kuwa chachu ya mabadiliko katika vituo vya kazi.

Naye Kaimu Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo, Bi. Mugage Mtani, amesema mafanikio ya chuo hicho yametokana na ushirikiano wa wadau mbalimbali ikiwa pamoja na Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Asasi zisizo za Serikali, Taasisi za Mafunzo ndani na nje ya nchi na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) - Malawi na Tanzania.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango amewapongeza wahitimu wote wa chuo hicho kwa kusoma kwa bidii na hatimae kutunukiwa vyeti na kuwataka wanaoendelea na masomo chuoni hapo kuiga mfano mzuri uliooneshwa na watangulizi wao.

**Imetolewa na;**

**Benny Mwaipaja**  
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Wizara ya Fedha na Mipango**